**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OSIFI YA RAIS - TAMISEMI**


Shule ya Sekondari Kalangalala,

S.L.P 508,
Geita.
19.04.2024

**Namba za simu**

**Mkuu wa shule; 0755354579**
**Makamu Mkuu wa shule; 0758505414/0712799199**
**Patron wa Shule; 0756737271/0766737271**


Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………….

S.L.P ………………………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KALANGALALA HALMASHAURI YA MJI GEITA MKOA WA GEITA**


1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka **2024/2025** tahasusi ya …………………… Shule ya Sekondari Kalangalala ipo kusini mwa stendi kuu ya mabasi yaendayo mikoani mita 100 toka stendi kuu kupitia lango la kutokea mabasi, vuka barabara ya rami utaona kibao cha shule. Nakutakia safari njema.

Muhula wa masomo unaanza tarehe **01/07/2024.** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 30/06/2024 mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/07/2024. Muda wa kuripoti ni kuanzia saa 4.00 asubuhi hadi 12.00 jioni tu.

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

2.1 Sare ya shule

a) Sare ya shule hii ni mashati mawili maupe (tetron) yenye mikono mirefu
b) Suruali mbili (02) dark blue yenye mifuko 3 angalia mfano wa kitambaa/mchoro/ fuata vipimo hauruhusiwi kushona suruali ya kubana (zinapatikana shuleni)




c) Sare ya michezo ni "Trak suit" yenye rangi ya dark blue yenye michirizi mieupe(inapatikana shuleni ), na raba jozi moja.
d) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi
e) Soksi jozi mbili nyeusi
f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi
g) Sweta moja la dark blue lenye michirizi mieupe shingoni na mikononi litakuwa na nembo ya shule (Linapatikana shuleni )



CamScanner

h) T.shirt 2 nyekundu zenye kola mikono mifupi zitakuwa na nembo ya shule (zinapatikana shuleni )
i) Nguo za kushindia (shamba dress) ni suruali nyeusi ya kitambaa
j) Tai yenye mistari ya dark blue na mieupe (Inapatikana shuleni ).
k) Jacket la dark blue lisilokuwa na kofia (kwa watakao hitaji kulingana na afya yako).
l) Gum– boot nyeusi (huvaliwa wakati wa mvua tu kwa watakaohitaji kulingana na eneo la shule lilivyo)
m) Picha 1 ya passport size ya mwanafunzi

**2.2. Michango Mbalimbali**

| S/ N | AINA YA MICHANGO | KIASI | AKAUNTI YA BENKI |
|---|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa Shule | 65,000/= | 31010026794 NMB Kalangalala Secondary school |
| 2 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= | |
| 3 | Tahadhari | 5,000/= | |
| 4 | Nembo ya shule | 5,000/= | |
| | **Jumla** | **80,000/=** | |

**Bima ya afya ni Tsh 50, 400/= inalipwa shuleni ofisi ya uhasibu tu na siyo kwenye akaunti ya Shule.**

**c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-**

i. Rimu NNE (4) A4 double A kwa mwaka.
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa taasusi ya PCB maalumu kwa somo la Biolojia.
iv. Scientific calculator kwa wanafunzi wa sayansi.
v. Godoro ft $2^1/_2$ X 6
vi. Mashuka pair 2 za rangi ya right bluu blanketi 1 nyepesi, mto na foronya yake ya right bluu 1, chandarua 1
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)
viii. Ndoo mbili 1 kubwa na 1ndogo zenye mifuniko
ix. Kwanja 1, jembe1, soft broom 1, mfagio wa nje1, hard broom 1, mopa 1 na reki 1.
x. Taulo 1
xi. Sanduku la chuma/ bati
xii. Kanda mbili kwa ajili ya kuogea tu
xiii. Sabuni, dawa za mswaki kwa matumizi binafsi
xiv. Mfuko wa kuwekea daftari
xv. Kidumu cha lita tano kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa
xvi. Daftari 10 za counter book quire 3 au zaidi, Faili moja na Result slip
xvii. Uje na picha za passport size 4 za wazazi na ndugu wengine wawili wanaoweza kumtembelea mwanafunzi.
xviii. Sabuni ya maji lita moja.

Mahitaji mengine hapo juu yanapatikana katika duka la Shule kwa bei nafuu kama vile; sare za shule (mafundi wapo wanashona suruali), godoro, mashuka, ndoo, vyombo vya kulia,neti, mafyekeo, jembe, mopa, mifagio, dissecting kit, soft broom, madaftari, kidumu cha maji ya kunywa, rimu, calculator n.k. Pia unapokuja kuripoti uje na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu.

..........................................................

GODFREY MAHEWA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KALANGALALA
GEITA



CS CamScanner

**KIAMBATANISHO NA.1**
**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI KALANGALALA**

Sheria hizi zinalenga kukupa **UTII, HESHIMA NA NIDHAMU**

Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kuling ana na ratiba ya shu Ie;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shu Ie;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**
Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuteni kwa namna yoyote lle, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

Mwanafunzi awapo shuteni atatakiwa kulala kwenye Sweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.

Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. **Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).



CS CamScanner

**SHERIA ZA MESINI**

- Lazima uwahi wakati wa chakula ili kuepuka kukosa chakula
- Usimwage chakula ovyo mezani na sakafuni
- Kila mwanafunzi aoshe vyombo vyake vya kulia chakula
- Usipige kelele wakati wa chakula
- Baada ya chakula ondoa mabaki yaliyodondoka mezani, chini kwa bahati mbaya
- Si ruhusa kujipikia
- Chakula cha wagonjwa kitashughulikiwa na viongozi wa Afya na wale wahusika
- Ni murufuku kuvaa ndala mesini

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla

(v) Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule

(vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(ix) Uvutaji wa sigara

(xi) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi

(xiii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana

(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

(xix) Kulala nje ya shule bila ruhusa

(xx) Kuja na pasi ya umeme au kutumia pasi ya umeme na mkaa bwenini

***Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

Mawasiliano kama kuna tatizo lolote yafanyike kupitia kwa viongozi wa wanafunzi, mwalimu wa zamu, bweni, madarasa na uongozi wa shule ili kuepusha migogoro shuleni. Unashauriwa muda wote kutumia busara ya kuzaliwa ili uweze kutenda na kuamua yaliyomema kwa kuzingatia sheria zote zilizoandikwa na yasiyoandikwa. "INAWEZEKANA TIMIZA WAJIBU WAKO"

Mimi………………………………………………………… wa kidato cha…………………………… nakubali kutii sheria na maagizo haya ya shule. Pindi nitakapovunja sheria na maagizo haya, hatua kali zichukuliwe kulingana na sheria na taratibu za shule.



CamScanner

Saini ya mwanafunzi_______________________________

Saini ya mzazi au mlezi_______________________________

Tarehe_______________________________

**KARIBU SANA SHULE HII**



CamScanner

# KIAMBATANISHO NO 2 TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

Unatakiwa kujaza sehemu zilizo wazi, aidha na kusoma kwa makini maelekezo yaliyoandikwa.

1. Majina matatu ya mwanafunzi
   …………………………………………………………………………………………
2. Anwani yako kamili……………………………………………………………………
3. Tarehe ya kuzaliwa mwezi na mwaka……………………………………………
4. Mahali ulipozaliwa
   …………………………………………………………………………………………
5. Dini au dhehebu…………………………………………………………………………
6. Uraia wako……………………………………………………………………………
7. Jina kamili la mzazi/mlezi wako……………………………………………………
8. Anwani ya mzazi/mlezi…………………………………………………………………
9. Namba ya
   nyumba…………………………………………………………………………………
10. Namba ya simu baba/mlezi……………………………
    Mama……………………………………………………
11. Mahali unapoishi Kitongoji…………………………………………
    mtaa…………………………………………
    Kata………………………………………… Wilaya……………………………

Mkoa……………………………

12. Jina la balozi wako…………………………………………….namba ya
    simu……………………………………
13. Andika namba za simu za ndugu au walezi wa karibu watatu tofauti na wazazi wanaoweza kukusaidia endapo wazazi/mlezi hawatapatikana ……………………………………………

Jina …………………………………namba ya simu……………………… uhusiano……………

Jina ………………………………… namba ya simu……………………… uhusiano……………

Jina …………………………………namba ya simu………………………uhusiano……………

Jina ………………………………… namba ya simu………………………uhusiano……………

Jina …………………………………namba ya simu………………………uhusiano……………



CamScanner

**AHADI**

Mimi………………………………………………………………… kwa utashi na akili yangu timamu ninaikubali nafasi ya masomo niliyopewa, nitakuwa tayari kujiendeleza kimasomo, nimezisoma na kuzielewa na nitazifuata sheria za shule pamoja na kanuni na taratibu zitakazotolewa.

Natambua kuwa nikifukuzwa shule kwa sababu ya kuvunja sheria za shule makusudi nitavunja moyo wa wazazi na walezi wote wanaonisaidia, ikiwemo serikali inayonisomesha, hivyo jamii itanidharau kabisa. Naahidi kuwa na utii kwa walimu na wafanyakazi wote waliopo hapa shuleni ili wanipende na kunisaidia zaidi. Sitakuwa tayari kuanzisha, kushauri wala kushiriki katika vurugu za aina yoyote hapa shuleni hususani mgomo kwani ni kwenda kinyume na sheria na taratibu za shule. Nitakuwa na utii na viongozi wa shule na upendo kwa wanafunzi wenzangu wote. Pia nitafanya bidii katika masomo na kazi zote za shule. Nitahudhuria vipindi vyote darasani bila kukosa katika siku zote za masomo na nitaomba ruhusa ninapopata shida.

**MUNGU NISAIDIE**

JINA NA SAINI YA MZAZI/MLEZI ______________________________

SAINI YA MWANAFUNZI ______________________________

TAREHE ______________________________



CS CamScanner

# GOVERNMENT OF TANZANIA
## MEDICAL EXAMINATION FORM:-

To medical officer ..................................................................................................................................

Mr/ Miss.............................................................................................................................. (Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a secondary education

(Day/boarding school)

1. Blood count ..........................................................................................................................
2. Stool examination.....................................................................................................................
3. Urine analysis .........................................................................................................................
4. Venereal disease .....................................................................................................................
5. T. B and leprosy test.................................................................................................................
6. Eye sight ...............................................................................................................................
7. Hearing..................................................................................................................................
8. Asthma..................................................................................................................................
9. Epilepsy.................................................................................................................................
10. Neuroses...............................................................................................................................
11. Pregnancy (girls) ....................................................................................................................
12. Speech..................................................................................................................................
13. Limbs...................................................................................................................................
14. Other serious Disease ..............................................................................................................

Remarks and additional information e.g. Physical defects or impediments, infection, chronic or family disease eg sickle cell.......................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

I certify that the above named student is fit/is not fit to pursue secondary education

Signature..............................................................................................................................

Designation ..........................................................................................................................

Station..................................................................................................................................

Date and stamp.......................................................................................................................



CS CamScanner